

**HOTUBA YA MAADHIMISHO YA SIKU YA MAZINGIRA  
DUNIANI ILIYOTOLEWA NA MHE: MKUU WA WILAYA  
YA MASASI TAREHE 05/06/2017 KATIKA KIJIJI CHA  
MKOLOPOLA KATA YA MKUNDI TARAFYA LULINDI**

**Viongozi na watendaji wa Chama na Serikali,  
Wananchi wote mabibi na mabwana,  
Itifaki imezingatiwa,**

Kwanza kabisa napenda kumshukuru mwenyezi **Mungu**,  
mwingi wa rehema kwa kutuweka hai hadi siku hii ya leo. Pia  
shukrani zangu ziende kwa viongozi, watendaji na wananchi  
wote wa kata hii kwa kushirikiana na kuweza kuandaa  
maadhimisho haya.

**Ndugu Wananchi,**

Siku ya mazingira duniani huadhimishwa kila tarehe 05/Juni  
ya kila mwaka. Maadhimisho haya yalianza tarehe 01/Juni  
na leo tarehe 05/Juni ndiyo kilele chake. Hivyo kwa siku tano  
mfululizo shughuli mbalimbali za uboreshaji wa mazingira  
kama vile kutoa elimu ya mazingira na kuhamasisha jamii  
kufanya usafi wa mazingira zimefanyika

## **Ndugu Wananchi,**

Kaulimbiu inayoongoza maadhimisho haya kimataifa ni **“Mahusiano Endelevu Kati ya Binadamu na Mazingira”**.

Kaulimbiu hii inahamasisha jamii kuwa na uhusiano endelevu na mazingira asilia ambapo kila mtu anapaswa kutambua, kufurahi, kujivunia na kulinda uzuri wa mazingira asilia yetu na kuhamasishana kuyatunza na kuyahifadhi.

Pamoja na kaulimbiu ya kimataifa, kaulimbiu yetu ya maadhimisho ya Siku ya Mazingira mwaka huu kitaifa ni **“Hifadhi ya Mazingira: Muhimili kwa Tanzania ya Viwanda.”** Kaulimbiu ya mwaka huu inatukumbusha tunapoelekea kwenye uchumi wa viwanda tuzingatie hifadhi ya mazingira. Mara nyingi tumeshuhudia katika uzalishaji wa viwanda mazingira asilia huharibiwa sana, hususan, kwa taka zitokanazo na uzalishaji na utupwaji wake. Kaulimbiu ya kitaifa inahimiza wazalishaji viwandani kuzingatia usimamizi endelevu wa taka zitokazo viwandani, uzalishaji wa bidhaa kwa viwango vinavyotakiwa na utumiaji endelevu wa bidhaa zinazozalishwa viwandani. Utiririshwaji ovyo wa maji machafu na utupaji ovyo wa taka za viwandani umepelekea kuwepo kwa uharibifu mkubwa wa mazingira asilia, hususan, ardhi na hewa.

## **Ndugu Wananchi**

Katika kutunza mazingira yetu ni muhimu kuzingatia mambo yafuatayo;

1. Kutochoma moto ovyo katika maeneo yote ya misitu na sehemu zenyewe uoto wa asili ili kutunza uoto wa asili na wanyama.
2. Kutokata miti ovyo ili kuepuka upotevu wa miti ya asili na isiyo ya asili. Na kila mwananchi anayehitaji kukata mti kwa ajili ya mbao katika eneo lolote ni lazima apate kibali halali cha serikali.
3. Kupanda na kutunza miti kuanzia ngazi ya kaya na katika taasisi zote za kiserikali na zisizo za kiserikali na maeneo mengine ya wazi katika jamii.
4. Kuepuka kilimo cha kuhamahama maana kilimo hiki kinasababisha ukataji miti ovyo na hivyo kusababisha jangwa na kupotea kwa viumbe hai pamoja na uoto wa asili
5. Kupata ushauri wa kitaalam katika shughuli zetu za kilimo ili kupata mazao ya kutosha na kuendelea kutunza rutuba katika ardhi.

6. Kutunza na kuzingatia usafi wa mazingira ili kujilinda na milipuko ya magonjwa mbalimbali ya kuambukiza hatimae kuwa na afya njema na kushiriki kikamilifu katika shughuli za kuzalisha mali.

## **HITIMISHO**

Kwa ujumla utunzaji wa mazingira ni swala mtambuka ambalo ni jukumu letu sote viongozi na wananchi kwa ujumla. Hapa nina maana ya viongozi wa serikali, vyama vyasiasa, dini, jadi na asasi nyingine za kijamii. Ninatoa wito kwa wamiliki wa viwanda na wazalishaji wa bidhaa za viwandani, pamoja na wananchi wote kwa ujumla kutumia fursa ya maadhimisho haya kuhakikisha maendeleo ya viwanda hayaathiri mazingira asilia ya Halmashauri yetu ambayo ni hazina ya vizazi vyasasa na vijavyo. Athari zinazotokana na uharibifu wa mazingira hazichagui dini, chama wala tabaka lolote katika jamii yetu. Hivyo tukishirikiana kwa pamoja tutafanikiwa.

## **MAZINGIRA SAFI!!!!!!**

**AHSANTE SANA KWA KUNISIKILIZA**